

VITU AMBAVYO HAVIHARIBU FUNGA.

1. Kuoga au kuogelea na kupata baridi kwa kujimwagia maji kutokana na joto.
2. Kula, kunywa, kufanya tendo la ndoa usiku mpaka kuingia kwa alfajir.
3. Kupiga mswaki mchana wa mwezi wa Ramadhan, bali inapendeza zaidi.
4. Kujitibu kwa dawa za halali isiwe dawa hiyo ni aina ya chakula, inafaa kuchoma sindano isiyo ya chakula, kuweka dawa ya jicho, dawa ya sikio hata kama kutapatikana aina ya utamu kwenye koo, ikiwa atachelewesha mpaka mwisho wa kufungua ni bora zaidi, lakini inafaa pia kutumia kifaa cha kuvuta katika kufungua mapafu kwa wenyewe Athma, haifunguzi kuonja kidogo chakula lakini kisifike kwenye koo, hakuna tatizo kusukutuwa na kuingiza maji puanili bila ya kupitiliza zaidi yasije yakaingia kooni na pia inafaa kutumia mafuta uzuri au kunusa mafuta uzuri.
5. wenyewe hedhi na Nifasi ikikatika damu wakati wa usiku inafaa kwao kuchewesha kuoga mpaka kuchomoza kwa alfajir na hivyo hivyo mwenye janaba.

UZINDUZI.

1. Atakaposilimu kafiri wakati wa mchana wa Ramadhan ni wajibu kwa kujizuia siku yake yote wala hata ilipa siku hiyo.
2. Hapana budi kwa mwenye kufunga kutia nia ya swaumu muda wowote usiku kabla ya kuchoza alfajir kwa swaumu ya faradhi, kwa swaumu nyingine kama vile swaumu ya siku sita za shawwal, swaumu ya arafa, swaumu ya ashura, ama swaumu za sunnah tu kama vile swaumu za siku tatu kila mwezi, anafaa kutia nia baada ya kuchomoza alfajir na hata kama jua litakuwa limechomoza na kupanda juu kiasi cha mkuki kwa sharti ya kuwa mtu hajakula.
3. Inapekezwa kuwa mwenye kufunga aombe dua wakati akiwa anafungua kwa kile alichokipenda kufungulia, Mtume (saw) anasema:

(Kwa hakika mwenye kufunga ana dua akiomba hairudi inakubaliwa) (Ameipokea Ibn Majah:1743).

Na mionganoni mwa dua zilizokuja kutoka kwa Mtume (saw) ni dua hii:

(Kiu kimeondoka na mishipa imelowa na ujira inshaallah umethibiti) (ameipokea Abu Daud: 2010)

4. Kujua kuingia kwa mwezi wa Ramadhani mchana wa siku hiyo ni wajibu mtu kujizuia na ni juu yake kuja kulipa.
5. Inapendekezwa kwa yule ambaye analo deni la kulipa basi afanye haraka kulilipa ili ajivue na dhima, na pia inafaa kuchelewesha, atawea kufunga mfululizo au kidogo kidogo, haifai kuchelewesha mpaka baada ya Ramadhan nyingine.